# الأسرة سكن ومودة

# HOTUBA YA IJUMAA.

## Familia Utulivu na Upendo

**Imefasiriwa na**

**Profesa\ Ayman Alasar**

**Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, mwenye kusema katika Kitabu chake Kitukufu:**

**{هُوَ الَّذِي خَلَقَكُم مِّن نَّفْسٍ وَاحِدَةٍ وَجَعَلَ مِنْهَا زَوْجَهَا لِيَسْكُنَ إِلَيْهَا}**

**{Yeye ndiye aliye kuumbeni katika nafsi moja; na katika hiyo hiyo akamfanya mwenzi wake, ili akae naye kwa utulivu}. Ninashuhudia kuwa hakuna Mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, ewe Mwenyezi Mungu tunakuomba peleka amani na baraka**

**juu yake na kwa Watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale waliowafuata kwa wema mpaka siku ya mwisho.**

**NA Baada ya Utangulizi:**

**Familia ndio msingi wa jamii, na ndio msingi wa ujenzi wake, kushikamana kwake na utulivu wake ndio kushikamana na kutulia kwa jamii, hivyo Uislamu umetoa uangalizi mkubwa wa kujenga family wa kufikiwa utulivu na upendo pamoja na huruma kwa wanafamilia wote, ambapo Anasema Mola Mtukufu:**

**{وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ}.**

**{Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika**

**katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanaofikiri}.**

**Mwenye kuzingatia katika Aya hii Tukufu anakuta kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka wazi kuwa ujenzi wa familia ni katika Alama zake kubwa, akafanya ndoa ni utulivu, hilo ni kwa vile mume anapata utulivu kwa mke wake na mke naye anapata utulivu kwa mume wake, kwani Mwenyezi Mungu amefanya upendo na huruma kuwa ni misingi ya ujenzi wa familia, kwani upendo ni sifa inayopelekea kushirikiana vizuri, kila mwanandoa anakuwa nguzo kwa mwengine, au kutafautiana kwa baadhi ya asili ambapo anasema Mtume S.A.W: "*Muumini wa kiume hambughudhi Muumini wa kike, ikiwa atachukia kwake tabia mbaya basi huridhia kwake tabia nyengine nzuri*", kwa sababu hiyo familia itakuwa yenye kusimama kwenye maana ya tabia njema na ushirikiano nzuri na huruma, na kupitia**

**familia hii iliyotulia na kushikana hukua mazuri na kuanzisha mambo mema na kizazi chema na kuenea furaha ndani ya nyumba.**

**Na kufikia utulivu na upendo ndani ya familia kunapaswa kujipamba na mambo:**

**Miongoni mwa mambo hayo: Kushirikiana vizuri na kuishi kwa wema ambapo Anasema Mola Mtukufu:**

**يقول تعالى: {وَعَاشِرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ}، ويقول نبينا (صلى الله عليه وسلم): (اسْتَوْصُوا بِالنِّسَاءِ خَيْرًا)، ويقول (صلى الله عليه وسلم): (خَيْرُ نِسَائِكُمْ مَنْ إِذَا نَظَرَ إِلَيْهَا زَوْجُهَا سَرَّتْه، وَإِذَا أَمَرَهَا أَطَاعَتْهُ، وَإِذَا غَابَ عَنْهَا حَفِظَتْهُ فِي نَفْسِهَا وَمَالِهِ).**

**Mwenyezi Mungu Anasema: {Na ishini nao kwa wema}, na anasema Mtume wetu Muhammad S.A.W: "*Wausieni wanawake mambo mema*" na anasema tena**

**Mtume S.A.W: "*Mke bora ni yule pindi anapoangaliwa na mume wake hufurahi, na pindi anapoamrishwa humtii, na anapokuwa mbali na mume wake humlindia kwenye nafsi yake na mali yake*".**

**Miongoni pia mwa hayo mambo: Mume kuhudumia familia yake kwa kuipatia huduma muhimu za chakula kinywaji na mavazi, ambapo Anasema Mola Mtukufu:**

**حيث يقول تعالى: {وَعَلَى الْمَوْلُودِ لَهُ رِزْقُهُنَّ وَكِسْوَتُهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ}، ويقول سبحانه: {لِيُنفِقْ ذُو سَعَةٍ مِّن سَعَتِهِ}، ويقول نبينا (صلى الله عليه وسلم): (أَفْضَلُ الصَّدقةِ مَا كَانَ عَنْ ظَهْرِ غِنًى، واليَدُ العُليا خيرٌ من اليَدِ السُّفلَى، وَابْدَأْ مَنَ تعولُ)، ويقول (صلى الله عليه وسلم): (كَفَى بِالْمَرْءِ إِثْمًا أَنْ يُضَيِّعَ مَنْ يَعُولُ).**

**{Na kwa watoto wanapaswa kupatiwa chakula chao na mavazi yao kwa wema} Anasema tena Mola Mtukufu:**

**{Mwenye nafasi atoe kiasi cha nafasi yake}. Na anasema Mtume wetu S.A.W: "*Sadaka bora ni inayobaki na kutosheleza kwa mtoaji, na mkono wa juu ni bora zaidi kuliko mkono wa chini, na anza kutoa kwa familia*".**

**Miongoni mwa mambo mengine: Kulinda siri kati ya wanandoa wawili, kwani kila mmjoa ni stara na utulivu kwa mwengine, hivyo kutoa siri ni jambo lisilo ridhiwa na dini wala na tabia njema, ambapo anasema Mtume wetu Muhammad S.A.W: "*Katika watu wenye nafasi mbaya mbele ya Mwenyezi Mungu siku ya kiyama, ni mume anayemfedhehesha mke wake na mke kumfedhehesha mume wake kisha siri zao zinasambaa na kuenea*".**

**Pia mambo mengine: Kushirikiana katika kulea watoto, na makuzi yaliyo sawa, wala haiishii nafasi ya mume na mke katika kulea watoto kwa kuwapa chakula na vinywaji tu bali ni zaidi ya hayo ikiwa ni pamoja na**

**kujenga misingi na maadili mema kwenye nafsi zao itakayowawezesha kusimama kwenye nafasi yao kwenye kuinua jamii na kuendeleza, na kwa hali hiyo wanakuwa ni kitulizo cha macho kwa baba zao na mama zao duniani na akhera, ambapo Anasema Mola Mtukufu:**

**{وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَزْوَاجِنَا وَذُرِّيَّاتِنَا قُرَّةَ أَعْيُنٍ وَاجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِينَ إِمَامًا}**

**{Na wale wanaosema ewe Mola wetu tupatie kutoka kwa wake zetu na vizazi vyetu kitulizo cha macho na utujalie tuwe viongozi kwa wacha-Mungu}. Na anasema Mtume S.A.W: "*Pindi anapofariki mwanadamu matendo yake yote hukatika isipokuwa hubakia mambo matatu: Sadaka endelevu, au elimu inayomnufaisha, au mtoto mwema anayemuombea duwa*", na kama inavyomaanishwa familia kwa kuwa na watoto lazima**

**iwe na maana ya haki za wazazi, ambapo Anasema Mola Mtukufu”**

**يقول الحق سبحانه: {وَقَضَى رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا}،**

**{Amehukumu Mola wako kutoabudiwa isipokuwa Yeye na wazazi wawili wafanyiwe wema}, hufikiwa usalama utulivu na furaha kwa wanafamilia.**

**Pia mambo mengine: Kushauriana kati ya wanafamilia katika mambo ya maisha, na hilo linapelekea kuhisi kila mmoja katika familia nafasi yake na umuhimu wake, na Mtume S.A.W alishauriwa na mke wake Ummu Salama R.A katika upatanishi wa Hudaibia na Mtume akakubali ushauri wa mkewe na kuuridhia, na ikawa ni kheiri kwenye ushauri wa mke wake. *Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe kake*.**

****

**Hotuba ya Pili:**

**Shukrani ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, swala na salamu zimwendee Nabii na Mtume wa mwisho naye ni Mtume Muhammad rehema na amani ziwe kwake pamoja na watu wake na Maswahaba zake wote.**

**Hakuna shaka kwa watu wa familia ya mume na mke kuwa na nafasi kubwa ya kulinda familia na kufikia utulivu wake, na hilo kupitia kuimarisha misingi ya upendo heshima utulivu na mapenzi kati yao, na kuzuia tafauti kwa kupeana nasaha na miongozo, ambapo Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:**

**حيث يقول تعالى: {وَقُل لِّعِبَادِي يَقُولُوا الَّتِي هِيَ أَحْسَنُ إِنَّ الشَّيْطَانَ يَنزَغُ بَيْنَهُمْ إِنَّ الشَّيْطَانَ كَانَ لِلْإِنسَانِ عَدُوًّا مُّبِينًا}، ويقول (عز وجل):**

{وَإِنْ خِفْتُمْ شِقَاقَ بَيْنِهِمَا فَابْعَثُوا حَكَمًا مِّنْ أَهْلِهِ وَحَكَمًا مِّنْ أَهْلِهَا إِن يُرِيدَا إِصْلَاحًا يُوَفِّقِ اللَّهُ بَيْنَهُمَا إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا خَبِيرًا}

**{Waambie waja wangu waseme maneno mazuri, maana shetani huchochea ugomvi kati yao. Hakika shetani ni adui aliye wazi kwa mwanadamu}. Na Anasema tena Mola Mtukufu: {Na mkichelea kutakuwapo mfarakano kati ya mke na mume basi pelekeni muamuzi kutoka jamaa za mume, na muamuzi kutoka jamaa za mke. Wakitaka mapatano Mwenyezi Mungu atawawezesha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye habari} hivi muna nini kwa baba zetu na watoto wetu wa kike na wale wenye ukaribu na sisi.**

**Sisi ni wenye kuhitaji sana kufikia utulivu na upendo kwenye nyumba zetu mpaka upendo uenee na utulivu ndani ya jamii yote.**

**Mola wetu tunakuomba utupatie kutoka kwa wake zetu na vizazi vyetu kitulizo cha macho na utujalie tuwe viongozi wa wacha-Mungu.**